

وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مَكْرُونَ وَعَيْلُوا الصَّلَاحَتِ لِيُسْتَخْلِفُنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا أَسْتَخْلَفْتُ  
الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ وَلَيُخْكِنَنَّهُمْ وَيَنْهَا اللَّهُ أَرْضَنِي لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُمْ مِنْ بَعْدِ حَرْقِهِمْ أَمَّا  
يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الظَّالِمُونَ



### Taarifa kwa Vyombo vya Habari

#### **Hao ndio Wanajeshi wa Misri, wa Kweli, na hivi ndivyo inavyopaswa kuwa Hasira yao kwa ajili ya Mwenyezi Mungu (Imetafsiriwa)**

Ummah unaendelea kuweka mifano bora kabisa ya kujitolea muhanga, ikithibitisha kwamba ni Ummah ulio hai ambaa unaweza kuugua lakini kamwe haufi na hauagi. Kila moto wa hasira unapopungua katika nyoyo za watu wake, wanyoofu huwasha cheche zake na kuwaangazia njia za Mto Nile dhidi ya wale walioasi dhidi ya Ummah wao, wakakiuka matukufu yake, wakanajisi sehemu zake takatifu, na kumwaga damu yake. Mnamo siku ya Jumamosi hii, tarehe 3/6/2023, mwanajeshi mmoja wa Misri aliyezasirika kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, Mtume Wake, na Dini yake, aliwashambulia wanajeshi wawili wa Kiyahudi na kuwaa, kisha akawashambulia wale waliokuja kuwatafuta na kumuua mmoja na kumjeruhi mwengine. Wayahudi walichukua hatua ya kutangaza kilichotokea huku wakiwa katika hali ya mshtuko. Hawakutarajia kwamba pigo lingewajia kutoka kwa wanajeshi wa Kimisri, ambao watawala wao wanatangaza kwamba misheni yao ni kulinda umbile la Kiyahudi. Kijana huyu aliwajia kutoka kwa usalama wao, akihuisha kumbukumbu ya Soliman Khattar na wengine ambaa waliwadhuru Mayahudi na kuzifurahisha nyoyo za Umma unaosononeka.

Ingawa hili lilikuwa ni tendo la mtu binafsi, sio tukio la kupita bali linaonyesha kile kinachotokota ndani ya nyoyo za wanajeshi katika hasira na kile ambacho wamejitarisha kufanya katika kukabiliana na yale ambayo Mayahudi wanawafanya watu wao huko Palestina. Yote haya yanaashiria kujitenga kwa watawala na utawala kutoka kwa wanajeshi na watu, na ye yote atakayeona sura ya fursa ataielekeza hasira yake kwenye ulemavu wa umbile hili lichukizalo, ambalo linanyenyeka kwa utawala huu shirikishi unaolinda umbile la Kiyahudi na kusimama baina ya watu na kuung'oa kwake, hata ikiwa ni kwa mikono yao mitupu. Basi, hali itakuwaje ikiwa utawala huu ungeng'olewa na njia ikawa wazi kwao kuikomboa Palestina yote? Je, hali ya Mayahudi ingekuwaje wakati huo?"

**Enyi watifu katika Jeshi la Kinanah**, jukumu lenu la kweli si kulilinda umbile la Kiyahudi, wala kuulinda utawala unaolilinda, wala kujishughulisha na biashara, kilimo, au kero zingine kutokana na dori yenu halisi ambayo serikali hii inakuvutieni kwayo kuitia rushwa na ufisadi, Mwenyezi Mungu akulindeni na hayo. Wajibu wenu wa kweli ni kuulinda Ummah na matukufu yake. Vipi matukufu yake yanaweza kukiukwa na ardhi yake kunyakuliwa na hali ndani yenu kuna mshipa unaopuma? Mtakutana pipi na Mwenyezi Mungu na hali hukmu zake zinapuuzwa na Dola yake, ambayo inalea na kulinda matukufu yenu, haipo, wakati nyinyi ni kizazi cha Fatihina (wafunguzi) wakubwa? Basi fuateni nyayo za babu zenu, inusuruni Dini yenu, na mumridhishe Mwenyezi Mungu kwa kuwanusuru wale wanaofanya kazi ya kutabikisha Dini yake na kusimamisha dola yake.

**Enyi wenge iklasi katika Jeshi la Kinanah**, kijana huyu shujaa na wengi kama yeye mionganini mwenu wanawaka hasira kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, matukufu yake, na maeneo yake matukufu, na hakuna kinachosimama baina yao na nusra yao kwa Uislamu isipokuwa utawala huu shirika. Njia sahihi ya kuikomboa Palestina inaanza kwa kuung'oa utawala huu kutoka kwenye mizizi yake, pamoja na ala na nembo zake zote, na kuutabikisha kwa upana na kwa ukamilifu Uislamu ndani ya Khilafah yake Rashida kwa njia ya Utume. Hili litanyanya Raya (bendera) ya jihad, kukomboa ardhi, na kuhuisha urithi wa Makhalifa watukufu kama vile Harun al-Rashid na al-Mu'tasim, wale wanaoitikia wito na kucasirika kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, na hivyo hasira zao huwa ni ufunguzi na ushindi. Tunamuomba Mwenyezi Mungu awape ushindi wanajeshi wanyoofu wa Misri na awajaalie kuwa wasimamishaji wa dola yake. Allahumma Amin.

[وَالَّذِينَ آمَنُوا وَهَاجَرُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَالَّذِينَ آوَوْا وَنَصَرُوا أُولَئِكَ هُمُ الْمُؤْمِنُونَ حَقًا لَهُمْ مَغْفِرَةٌ وَرِزْقٌ كَرِيمٌ]

"Na walio amini wakahama na wakapigana Jihadi katika Njia ya Mwenyezi Mungu, na walio toa mahala pa kukaa na kuwanusuru, hao ndio Waumini wa kweli. Watapata msamaha wa Mwenyezi Mungu na kuruzukiwa kwema." [Al-Anfal:74]

Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir katika Wilayah Misri

Tovuti Rasmi ya Hizb ut Tahrir:

Tovuti: [www.hizb.net](http://www.hizb.net)

[www.hizb-ut-tahrir.org](http://www.hizb-ut-tahrir.org)

Pepe: [info@hizb.net](mailto:info@hizb.net)

Tovuti ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir:

[www.hizb-ut-tahrir.info](http://www.hizb-ut-tahrir.info)